

# Je, unasubiri matokeo ya kipimo cha COVID-19?

Ilibadilishwa 11/16/2020

Leo ulipimwa COVID-19. Huenda ikachukua siku chache kupata matokeo yako. Matokeo ya kipimo cha leo yatakuonyesha ikiwa umeambukizwa au unaugua leo. Inawezekana unaweza kupatikana na virusi katika siku zijazo.

## Wakati unasubiri matokeo:

- Ikiwa unapimwa kwa sababu una dalili za COVID-19, umetangamana kwa karibu na mtu aliye na COVID-19, au ulipendekezewa upimwe, **kaa nyumbani na usiende nje kwa umma, hata kama huhisi kuugua.** Kukaa nyumbani kutazuia COVID-19 kuenea.
- Ikiwa unahitaji kuona mtoa huduma ya afya, mpigie simu kwanza na umweleze kuwa ulipimwa COVID-19 na unasubiri matokeo.

## Ikiwa matokeo yako ya kipimo yanaonyesha una virusi, fanya mambo haya mara moja:

- **Kaa nyumbani** na mbali na watu wengine, ikiwa ni pamoja na watu ambao unaishi nao.
- **Unda orodha ya majina na nambari za simu za watu uliotangamana nao kwa karibu.** Mtu uliyetangamana naye kwa karibu ni mtu ambaye ulikuwa karibu naye umbali wa chini ya futi 6 kwa jumla ya dakika 15 au zaidi kwa kipindi cha saa 24 wakati wa kipindi chako cha uwezekano wa kuambukiza. Kipindi chako cha uwezekano wa kuambukiza huanza siku mbili kabla ya dalili kuanza - au siku mbili kabla ya tarehe uliyopimwa ikiwa huna dalili.  
Wafanyakazi wa Idara ya Afya watakuomba maelezo haya wakati watakupigia simu na watawapa maelezo muhimu watu mliotangamana nao kwa karibu kuhusu jinsi ya kuzuia ueneaji zaidi. Huenda wafanyakazi wa Idara ya Afya wasikupigie mara moja, kwa hivyo chukua hatua na uwasiliane na watu uliotangamana nao kwa karibu ikiwa ungependa kufanya hivyo. Watu uliotangamana nao kwa karibu wanapaswa kujiweka karantini (kukaa nyumbani na mbali na watu wengine kwa siku 14), na kufikiria kuhusu kupimwa.
- **Wasiliana na mtoa huduma wako wa afya ikiwa unahitaji** kuzungumza kuhusu utunzaji na matibabu yako ya dalili zozote.
- **Jibu simu ikiwa unapigiwa simu na Idara ya Afya.** Mtu anayekupigia atakupata maelezo muhimu. Ukikosa simu, unaweza kutupigia tena kupitia 802-863-7240.

## Ikiwa matokeo yako ya kipimo yanaonyesha huna virusina uko katika karantini kwa sababu ya kusafiri au kutangamana kwa karibu na mgonjwa wa COVID-19 na:

- ulipimwa katika **siku ya 7** ya karantini au baadaye, na huna dalili yoyote, **unaweza kumaliza karantini.**  
AU
- ulipimwa **kabla ya siku ya 7** ya karantini, **kaa katika karantini** hadi upate matokeo ya kuonyesha huna virusi katika au baada ya siku ya 7, au kwa muda wote wa karantini ya siku 14.

## Au, ikiwa matokeo ya kipimo chako ni hasi na hujajiweka karantini kwa sababu ya kusafiri au kutangamana kwa karibu na mtu aliye na COVID-19:

- endelea kuchukua hatua za kujizuia kama vile kuvaa barakoa, kunawa mikono na kudumisha umbali wa kimwili.
- ikiwa unaugua maradhi mengine isipokuwa COVID-19, kaa nyumbani hadi dalili zitakapopata nafuu.

**Kwa maelezo zaidi kuhusu COVID-19: [www.healthvermont.gov/COVID-19](http://www.healthvermont.gov/COVID-19)**

Swahili

## Unachohitaji kufanya ikiwa umekuwa karibu sana na mtu ambaye ametambuliwa kuwa COVID-19

Maelezo haya ni kwa watu ambao walitangamana kwa karibu sana na mtu ambaye ana COVID-19. Kutangamana kwa karibu kunamaanisha kuwa katika ukaribu wa futi sita au mita mbili kwa dakika 15 au zaidi katika kipindi cha saa 24 wakati mtu huyo alikuwa na uwezo wa kuambukiza, kipindi ambacho huanza siku mbili kabla ya dalili zozote kuonekana (au kwa watu wasio na dalili yoyote, siku mbili kabla ya siku waliyopimwa) na kinaendelea mpaka [atakapopona](#). Kutangamana kwa karibu hakumaanishi kuwa katika umbali wa zaidi ya futi sita au mita mbili katika mazingira sawa ya ndani kwa chini ya dakika 15, kutembea karibu na, au kuwa katika chumba kimoja kwa muda mfupi. Wafanyakazi wa huduma za afya: tafadhali tazama [“COVID-19: Nini cha kufanya ikiwa wewe ni mfanyakazi wa huduma za afya”](#).

Mifano ya kutangamana	Mifano ya KUTOTANGAMANA
Unaishi katika nyumba moja	Ulikuwa keshia wake katika duka la vyakula
Ninyi ni wenzi wa karibu	Wewe ni mfamasia uliyempa mtu huyu dawa
Mliabiri gari moja wakati mtu huyo alikuwa na uwezo wa kuambukiza	Ulikuwa mbele ya mtu huyu katika foleni ya duka

### Kaa katika karantini nyumbani na ufuatilie dalili kwa siku 14:

- Siku ya 0 ni siku ambayo ulikuwa karibu sana na mtu aliyeambukizwa mara ya mwisho.
- Angalia iwapo una dalili, hata ikiwa sio kali, za kikohozi, upungufu wa pumzi au tatizo la kupumua, homa, kibaridi, kutetemeka mara kwa mara na kibaridi, uchovu, maumivu ya misuli au maumivu ya mwili, kuumwa kwa kichwa, kuwashwa kooni, kupoteza kupya kwa ladha au harufu, kuziba au kamasi kwenye pua, kichefuchefu au kutapika, au kuhara.
- Usiondoke nyumbani, isipokuwa kwa ajili ya kupata huduma ya matibabu. [Vaa barakoa ya kitambaa](#) ikiwa unahitaji kuondoka nyumbani.
- Piga simu kabla ya kutembelea mtoa huduma za afya au idara ya dharura.
- Ikiwezekana, kaa katika chumba mahususi nyumbani kwako na utumie bafu na choo tofauti.
- Kaa angalau futi sita au mita mbili mbali na watu wengine nyumbani kwako wakati wote. Vaa barakoa ya kitambaa ikiwa uko katika chumba chochote na watu wengine, isipokuwa ikiwa unashindwa kupumua. Usitumie vifaa vya nyumbani na wengine.
- Endelea kuwasiliana na wengine - tumia teknolojia ili uwasiliane na marafiki na familia.

Ikiwa baada ya siku 14 bado huna dalili, unaweza kuacha kukaa katika karantini. Kipimo cha matokeo hasi ya COVID-19 wala barua kutoka Idara ya Afya hazipaswi kuhitajika na mwajiri wako ili urudi kazini. Idara ya Afya haitoi barua zinazoonyesha kuwa unaweza kurudi kazini.

### Usafishaji na uoshaji wa kila siku:

- Safisha na utumie kemikali ya kuua viini vya maradhi kwenye nyuso katika nyumba yako. Ikiwa unakaa katika chumba tofauti na unatumia bafu na choo tofauti, osha vyumba hivi mwenyewe. Muombe mtu mwingine asafishe maeneo mengine ya nyumbani.
- Osha kabisa vifaa vya nyumbani, kama vile vyombo vya jikoni, baada ya kuvitumia.
- Nawa mikono yako mara kwa mara kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20. Tumia kieuzi cha mikono kilicho na kileo iwapo huna sabuni na maji.

**Ikiwa wakati wowote unaonyesha dalili:**

- Wasiliana na mtoa wako wahuduma za afya kwa simu ili kujua ikiwa unapaswa kutathminiwa. Mjulisha kuwa uko katika karantini nyumbani kutokana na virusi vipya vya corona kwa sababu umetangamana kwa karibu na mtu ambaye ametambuliwa kuwa na COVID-19.
- Ikiwa unahitaji dharura ya matibabu, piga 9-1-1 au nenda hospitalini.
- Ikiwa huna mtoa huduma, piga simu 2-1-1 ili uunganishwe na kliniki katika eneo lako.
- Watu walio na maradhi yasiyo makali wanaweza kutibu dalili zao nyumbani: kupumzika kwa muda mrefu, kunywa viowevu vingi, na kutumia dawa za kupunguza makali ya homa ikiwa inahitajika.

**Wakati wa kupata huduma ya matibabu mara moja:**

Ikiwa una matatizo ya kupumua, maumivu ya kifua, kuchanganyikiwa, au mabadiliko ya rangi kwenye midomo, ufizi, uso, karibu na macho au kucha zako, tafuta huduma ya matibabu mara moja. Unapopiga simu kwa ajili ya huduma ya matibabu, mjulishe mtoa huduma au 9-1-1 kuwa uko kwenye karantini nyumbani kwa sababu umetangamana kwa karibu na mtu aliye na COVID-19.

**Tofauti kati ya kujitenga na karantini**

	<b>Kujitenga mwenyewe</b>	<b>Kujiweka katika karantini</b>
Inapaswa kuwa kwa nani?	Watu walio na dalili za COVID-19 <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kwa watu walio na COVID-19 ambao sio wagonjwa vya kutosha kulazwa hospitalini, <b>au</b></li> <li>• Kwa watu ambao wanasubiri matokeo ya kipimo</li> </ul>	Watu wasio na dalili za COVID19 <ul style="list-style-type: none"> <li>• Watangamani wa karibu na watu walio na COVID19</li> </ul>
Kwa muda gani?	Hadi upone, ambao ni wakati yote matatu yametokea (isipokuwa kama utapata maagizo tofauti kutoka kwa mtoa huduma wako wa matibabu): <ol style="list-style-type: none"> <li>1. Imekuwa masaa 24 ya kutokuwa na homa na bila kutumia dawa za kupunguza homa, na</li> <li>2. Dalili zingine zimepungua, na</li> <li>3. Angalau siku 10 zimepita tangu dalili zako zilipoonekana kwanza.</li> </ol> Au ikiwa hukuwa na dalili wakati ulipimwa, kupona ni wakati siku 10 zimepita tangu tarehe ya kipimo chako cha kwanza chenye matokeo ya kuonyesha una virusi na ulipoendelea kutokuwa na dalili.	Kwa siku 14 tangu tarehe ya mwisho ya uwezekano wa kuwa katika hatari. Siku uliyokuwa katika hatari ni Siku ya 0.  Una chaguo la kupimwa wakati wa kipindi chako cha karantini ikiwa hujapata dalili zozote. Katika siku ya 7 au baada ya siku 7, unaweza kupimwa kupitia kwa mtoa huduma wako au kwenye kituo cha muda cha upimaji. Kaa katika karantini hadi utakapokea matokeo yako. Ikiwa matokeo ni hsi, na bado huna dalili zozote, unaweza kuacha kukaa katika karantini. Utapata simu kutoka Idara ya Afya wakati matokeo yako yanapokuwa tayari, ambayo kwa kawaida ni kati ya siku 2-4, au mapema. Pia utapokea barua katika sanduku lako katika siku 7 baada ya kupimwa.
Hii inamaanisha nini?	Ukae nyumbani 24/7 katika chumba tofauti ndani ya nyumba, utumie bafu na choo tofauti, uepuke kuwa karibu na wengine. Vaa barakoa ikiwa uko kwenye chumba na watu wengine, isipokuwa ikiwa unashindwa kupumua.	Ukae nyumbani 24/7, ukifuatilia dalili, na ukidumisha umbali wa kutengana. Ikiwezekana, tumia chumba, bafu na choo tofauti. Ikiwa unaonyesha dalili, watu ambao wametangamana nawe kwa karibu pia wanapaswa kujitenga.

Maelezo zaidi yanapatikana katika tovuti yetu: [www.healthvermont.gov/COVID-19](http://www.healthvermont.gov/COVID-19)

## Unachostahili kufanya ukitambuliwa kuwa na COVID-19

### Jitenge nyumbani:

- Usiondoke nyumbani, isipokuwa kwa ajili ya kupata huduma ya matibabu. Piga simu kabla ya kumtembelea mtoa huduma ya afya au idara ya dharura na uvae [barakoa ya kitambaa](#).
- Watu wengi walio na maradhi yasiyo makali wanaweza kupona wakiwa nyumbani. Ingawa hakuna matibabu mahususi ya COVID-19, unapaswa kupumzika kwa muda mrefu, kunywa viowevu vingi, na kutumia dawa za kupunguza makali ya homa ikiwa inahitajika.
- Kadri iwezekanavyo, kaa katika chumba mahususi ndani ya nyumba yako na utumie choo na bafu tofauti. Kaa angalau futi sita au mita mbili mbali na watu wengine nyumbani kwako wakati wote. Vaa barakoa ya kitambaa ikiwa uko kwenye chumba na watu wengine, isipokuwa ikiwa unashindwa kupumua. Usitumie vifaa vya nyumbani pamoja na wengine.
- Kuwa na mtu mwingine wa kutunza wanyama vipenzi wako. Idadi ndogo ya wanyama vipenzi wameripotiwa kuugua COVID-19. Watu wenye virusi wanapaswa kuepuka kutangamana na wanyama hadi taarifa zaidi zifahamike. Ikiwa unahitaji kushughulikia mnyama kipenzi wako, vaa barakoa ya kitambaa na unawe mikono yako kabla na baada ya kumshughulikia.
- Endelea kuwasiliana na wengine - tumia teknolojia ili uwasiliane na marafiki na familia.

### Usafishaji na uoshaji wa kila siku:

- Safisha na utumie kemikali ya kuua viini vya maradhi kwenye chumba na choo chako tofauti. Muombe mtu mwingine asafishe maeneo mengine ya nyumbani kwako.
- Osha kabisa vifaa vya nyumbani, kama vile vyombo vya jikoni, baada ya kuvitumia.
- Nawa mikono yako mara kwa mara kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20. Tumia kieuzi cha mkono kilicho na kileo iwapo huna sabuni na maji.

### Wakati wa kupata huduma ya matibabu mara moja:

Ikiwa una matatizo ya kupumua, maumivu ya kifua, kuchanganyikiwa, au mabadiliko ya rangi kwenye midomo, ufizi, uso, karibu na macho au kucha zako, tafuta huduma za matibabu mara moja. Unapopiga simu kwa ajili ya huduma ya matibabu, eleza mtoa huduma au 911 kwamba una COVID-19 na unajitenga nyumbani.

### Watu ambao wametangamana nawe kwa karibu wakati ulianza kuwa na uwezekano wa kuambukizana wanapaswa wanapaswa kujiweka katika karantini nyumbani - hata kama hawana dalili:

- Watu ambao walitangamana nawe katika kipindi ulipoanza kuwa na uwezekano wa kuambukizana, ambacho huanza siku mbili kabla ya kupata dalili zozote (au ikiwa huonyeshi dalili zozote, siku mbili kabla ya wewe kupimwa) na kinaendelea hadi [unapopona](#), wanapaswa kuwa kwenye karantini nyumbani. Wanaweza kurejelea mwongozo wa [“Unachofaa kufanya ikiwa umetangamana kwa karibu na mtu ambaye ametambuliwa kuwa na COVID-19”](#). Watangamani wa karibu na watangamani wako hawahitajiki kufuata mwongozo (isipokuwa kama wanaonyesha dalili).
- Kutangamana kwa karibu kunamaanisha kuwa katika ukaribu wa futi sita au mita mbili kwa dakika 15 au zaidi katika kipindi cha saa 24. Kutangamana kwa karibu hakumaanishi kuwa katika umbali wa zaidi ya futi sita au mita mbili katika mazingira sawa ya ndani kwa chini ya dakika 15, kutembea karibu na, au kukaa katika chumba kimoja kwa muda mfupi.

Mifano ya kutangamana	Mifano ya KUTOTANGAMANA
Watu wanaoishi katika nyumba moja	Keshia kwenye duka la vyakula
Wenzi wa karibu	Wafamasi waliokupa dawa
Watu ambao waliabiri gari moja nawe wakati ulikuwa na uwezo wa kuambukiza	Mtu aliye mbele yako katika foleni ya dukani

**Ni salama kuacha kujitenga nyumbani wakati umepona. Isipokuwa kama utapata maagizo tofauti kutoka kwa mtoa huduma wako wa matibabu, kupona ni wakati mambo yote matatu yametokea:**

1. Imekuwa masaa 24 ya kutokuwa na homa bila kutumia dawa za kupunguza makali ya homa, na
2. Dalili zingine zimepungua, na
3. Angalau siku 10 zimepita tangu dalili zako zilipoonekana kwanza.

**Au** ikiwa hukuwa na dalili wakati ulipopimwa, kupona ni wakati siku 10 zimepita tangu tarehe ya kipimo chako cha kwanza chenye matokeo ya kuonyesha una virusi na ulipoendelea kutokuwa na dalili.

Kipimo cha matokeo hasi ya COVID-19 wala barua kutoka Idara ya Afya hazipaswi kuhitajika na mwajiri wako ili urudi kazini. Hatutoi barua zinazoonyesha kuwa unaweza kufanya kazi.

### Tofauti kati ya kujitenga na karantini

	Kujitenga mwenyewe	Kujiweka katika karantini
Inapaswa kuwa kwa nani?	Watu walio na dalili za COVID-19 <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kwa watu walio na COVID-19 ambao sio wagonjwa vya kutosha kulazwa hospitalini, <b>au</b></li> <li>• Kwa watu ambao wanasubiri matokeo ya kipimo</li> </ul>	Watu wasio na dalili za COVID-19 <ul style="list-style-type: none"> <li>• Watu ambao wamekuwa karibu sana na watu walio na COVID-19</li> </ul>
Kwa muda gani?	Hadi upone, ambao ni wakati yote matatu yametokea (isipokuwa kama utapata maagizo tofauti kutoka kwa mtoa huduma wako wa matibabu): <ol style="list-style-type: none"> <li>1. Imekuwa masaa 24 ya kutokuwa na homa na bila kutumia dawa za kupunguza homa, na</li> <li>2. Dalili zingine zimepungua, na</li> <li>3. Angalau siku 10 zimepita tangu dalili zako zilipoonekana kwanza.</li> </ol> <p>Au ikiwa hukuwa na dalili wakati ulipimwa, kupona ni wakati siku 10 zimepita tangu tarehe ya kipimo chako cha kwanza chenye matokeo ya kuonyesha una virusi na ulipoendelea kutokuwa na dalili.</p>	Kwa siku 14 tangu tarehe ya mwisho ya uwezekano wa kuwa katika hatari. Siku uliyokuwa katika hatari ni Siku ya 0. Una chaguo la kupimwa wakati wa kipindi chako cha karantini ikiwa hujapata dalili zozote. Katika siku ya 7 au baada ya siku 7, unaweza kupimwa kupitia kwa mtoa huduma wako au kwenye kituo cha muda cha upimaji. Kaa katika karantini hadi utakapopokea matokeo yako. Ikiwa matokeo ni hsi, na bado huna dalili zozote, unaweza kuacha kukaa katika karantini. Utapata simu kutoka Idara ya Afya wakati matokeo yako yanapokuwa tayari, ambayo kwa kawaida ni kati ya siku 2-4, au mapema. Pia utapokea barua katika sanduku lako katika siku 7 baada ya kupimwa.
Hii inamaanisha nini?	Ukae nyumbani 24/7 katika chumba tofauti ndani ya nyumba, utumie bafu na choo tofauti, uepuke kuwa karibu na wengine. Uvae barakoa ikiwa unahitaji kuwa katika chumba kimoja na watu wengine, isipokuwa ikiwa unashindwa kupumua.	Ukae nyumbani 24/7, ukifuatilia dalili, na ukidumisha umbali wa kutengana. Ikiwezekana, tumia chumba, bafu na choo tofauti. Ikiwa unaonyesha dalili, watu ambao wametangamana nawe kwa karibu pia wanapaswa kujitenga.

**Maelezo zaidi yanapatikana katika tovuti yetu: [www.healthvermont.gov/COVID-19](http://www.healthvermont.gov/COVID-19)**

Mwongozo huu uliundwa na afya ya umma na wataalamu wa afya kwa kutumia kanuni zilizoithibitishwa za afya ya umma wakati huu ambapo maambukizi ya virusi vinavyosababisha maradhi ya COVID-19 katika jamii ya Vermont ni ya kiwango cha chini sana. Unaweza kurekebisha kulingana na mabadiliko ya hali za eneo na jimbo.

### Je, kutafanyika nini iwapo mtoto wangu ana dalili akiwa nyumbani au augue akiwa shuleni?

- Iwapo mtoto wako ana baadhi ya dalili zilizoordheshwa hapo chini, mwache akae nyumbani na asiende shuleni na uwasiliane na shule ili uripoti kutokuwepo kwake.
- Iwapo mtoto wako ana dalili zozote zilizoordheshwa hapo chini akiwa shuleni, atapelekwa katika eneo lililotengwa mahususi kwa wanafunzi wasiojihisi vizuri na utapigiwa simu uje kumchukua mtoto wako haraka iwezekanavyo.
- Tunakuhimiza utie saina fomu ya kutoa idhini ambayo inakubalisha kushirikiwa kwa maelezo kati ya mwuguzi wa shule ya mtoto wako (ikiwa anapatikana) na mtoa huduma za kiafya wakati mtoto wako anaugua.
- Huku ikihimizwa sana kuwa maamuzi kuhusu wakati mwanafunzi anaweza kurudi shuleni yafanywe na mwuguzi wa shule, mtoa huduma za afya wa mwanafunzi, na familia, maamuzi kama haya ni lazima yatakikishe kabisa afya na usalama wa shule na jamii ya mtoto wako.

### Je, ni lini mtoto wangu anahitaji kupimwa COVID-19?

Kikohozi (kipya)	Iwapo mtoto wako ana <b>MOJAWAPO</b> ya dalili hizi, inawezekana <b>anahitaji kupimwa COVID-19</b> .
Upungufu wa pumzi au kushindwa kupumua	
Ukosefu wa hisia za ladha (mpya)	
Ukosefu wa hisia za harufu (mpya)	
Homa pekee inayoendelea > saa 24 (halijoto ya zaidi ya 100.4°)	
Homa(halijoto ya zaidi ya 100.4°)	Iwapo mtoto wako ana dalili hizi <b>MBILI AU ZAIDI</b> , <b>ANAWEZA kuhitajika apimwe COVID-19</b> .
Kibaridi	
Maumivu ya misuli au mwili	
Maumivu ya kichwa	
Mwasho wa koo	
Uchovu mwingi	
Kuziba au kuwa na kamasi puani (mpya)	
Kichefuchefu au kutapika	
Kuendesha	



## Je, mtoto wangu anaweza kurudi shuleni wakati gani?

**Huhitaji** barua iliyo na saini ya daktari ili mtoto wako arudi tena shuleni.

- Iwapo mtoto wako **amepimwa COVID-19**:
  - Lazima awekwe katika karantini hadi apokee matokeo ya kipimo chake.
  - Iwapo matokeo ya kipimo yanaonyesha **HANA VIRUSI**, mtoto wako anaweza kurudi shuleni baada ya:
    - Kukosa kuwa na homa kwa saa 24 bila kutumia dawa za kupunguza homa. **NA**
    - Kujihisi kupata nafuu, **nadalili** zake kupungua.
  - Iwapo matokeo ya kipimo yanaonyesha **ANA VIRUSI**, anaweza kurudi shuleni baada ya:
    - Kukosa kuwa na homa kwa saa 24 bila kutumia dawa za kupunguza dalili za homa, **NA**
    - Kupunguka kwa dalili nyingine, **NA**
    - Kuisha kwa angalau siku 10 tangu kutokea kwa dalili zozote.
- Iwapo mtoto wako **hakupimwa** COVID-19 kwa sababu alikuwa na moja tu ya dalili zilizopo katika kijisanduku cha manjano kilicho hapo juu, anaweza kurudi shuleni iwapo:
  - Hajakuwa na homa kwa saa 24 bila kutumia dawa za kupunguza dalili za homa **NA**
  - Amehisi kupata nafuu kwa angalau saa 24 (dalili zimepungua au zimeisha).
- Iwapo mtoto wako amekuwa na dalili iliyoko katika kijisanduku chekundu au dalili mbili au zaidi katika kijisanduku cha manjano lakini hakuchunguzwa na mtaalamu wake wa kiafya na hakupimwa COVID-19, anaweza kurudi shuleni baada ya:
  - Kukosa kuwa na homa kwa saa 24 bila kutumia dawa za kupunguza homa, **NA**
  - Dalili zingine kupungua, **NA**
  - Kuisha kwa angalau siku 10 tangu kutokea kwa dalili zozote.

Hati hii ilipitishwa kwa ruhusa kutoka kwa [Idara ya Afya ya Rhode Island](#)

[COVID-19 katika Watoto Wanaouguua \(Pre-K – Darasa la 12\) Mchakato wa Haraka wa Kuchunguza Wagonjwa, Utathmini, Upimaji na Kurudi Shuleni](#)

[Mwanzo Thabiti na Wenye Afya: Mwongozo wa Usalama na Afya wa Shule za Vermont](#)